**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**621** **KISWAHILI**

**Muda: Saa 3.** **Jumatatu, 04 Mei 2009 mchana**

---

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu **B** and **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Toa hoja nne zinazoonyesha nafasi ya methali katika kuelimisha jamii.
2. Eleza sifa nne za hotuba nzuri ya Kiswahili.
3. Eleza mambo manne ya kuzingatia unapofundisha somo la sarufi.
4. Toa faida nne za ushairi wa Kiswahili kwa wanafunzi wa shule.
5. Eleza umuhimu wa maandiko ya Kiswahili katika kukuza lugha.
6. Taja mambo manne muhimu yanayoweza kujitokeza katika maandalio ya somo.
7. Eleza mchango wa nyimbo katika kufundisha maadili.
8. Toa hoja nne za kuthibitisha faida za mbinu shirikishi darasani.
9. Eleza nafasi ya lugha ya Kiswahili katika kukuza utamaduni wa Mtanzania.
10. Tofautisha kati ya hadithi na riwaya kwa hoja nne.

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. Eleza kwa hoja tano faida za kushirikisha wanafunzi katika michezo ya lugha.
12. Toa hoja tano za umuhimu wa vitabu vya fasihi kwa maendeleo ya mwanafunzi.
13. Jadili nafasi ya kazi za tungo za Kiswahili katika kuimarisha mshikamano wa kijamii.
14. Eleza hatua nne za mwalimu anapopanga shajara ya kazi za kila siku.

## SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

15. Toa sifa tano za mwalimu bora wa somo la Kiswahili.

16. Eleza faida tano za kufundisha kwa kutumia mijadala.

17. Jadili mbinu tano zinazomwezesha mwalimu kumudu darasa vyema.

18. Eleza mambo matano ya kuzingatia wakati wa kutunga maswali ya mtihani wa Kiswahili.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org